



**CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII UFUNDI MISUNGWI**  
**(MISUNGWI COMMUNITY DEVELOPMENT TECHNICAL TRAINING INSTITUTE)**  
S.L.P 2799 MWANZA | Barua pepe: [pmissungwi@jamii.go.tz](mailto:pmissungwi@jamii.go.tz)

---

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUFUNGULIWA KWA CHUO KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026**

Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi (Misungwi CDTTI) ni Chuo cha Serikali chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kipo Wilaya ya Misungwi Mkoani Mwanza na kimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa nambari **REG/EOS/015** na kupata ithibati kamili (Full Accreditation).

Chuo kinapenda kuutangazia umma kwamba kitafunguliwa rasmi tarehe **03 Novemba 2025 siku ya Jumatatu** na masomo yataanza tarehe **10 Novemba 2025**.

Mambo ya Kuzingatia wakati wa kuripoti Chuoni;

**MWAKA WA KWANZA (MAKAZI NI NDANI YA CHUO KIPAUMBELE KWA WASICHANA NA WAVULANA WATAKAOWAHI MAPEMA)**

1. Kuhakikisha kuwa umechaguliwa kujiunga na chuo na kupata msimbo (Code) utakaofika nao Chuo baada ya uhakiki na kwa waliochaguliwa na OR-TAMISEMI hawatakua na msimbo (Code)
2. Kuhakikisha kuwa una joining instructions (maelekezo ya kujiunga), fomu ya hospitali, vyeti halisi na nakala za vyeti vya shule na kuzaliwa
3. Kuwa na kiwango cha Ada kisichopungua 450,400/= (laki nne na elfu hamsini mia nne)
4. Utaratibu wa usajili ufuatwe kulingana na tangazo la usajili mara ufikapo chuoni
5. Kwa mwenye Bima ya AFYA NHIF afike nayo na nakala yake ili uhakiki ufanyike
6. NIDA NAMBA NI LAZIMA KWA KILA MWANACHUO

**KWA WANACHUO WANAOENDELEA NA MASOMO**

1. Usajili utafanyika kama unavyofanyika kwa mwaka wa kwanza zingatia muda wa kuripoti na usiingie darasani mpaka ukamilishe usajili.
2. Hakikisha umelipa madeni ya ada ya nyuma kabla ya kufika chuoni tarehe ya kufunguliwa
3. Wanaohitaji makazi ya ndani ya Chuo **kwa wanaume tu** walipe ada kabla ya kufika chuoni ili nafasi zao ziweze kuhifadhiwa (Nafasi zilizopo ni chache tu). Wanawake wote wataishi ndani ya Chuo.
4. Hakikisha umelipa ada ya muhula wa kwanza walau kiwango cha Chini 450,400/=

Kwa wanachuo wote usajili utafanyika kwa njia ya mtandao mara ufikapo chuoni

Chuo kinatoa wito kwa Wanachuo wote kuzingatia tarehe ya kufungua chuo na tarehe ya mwisho ya Usajili ambayo ni tarehe **21 Novemba 2025** Kwa atakayechelewa baada ya tarehe hiyo atakuwa amepoteza nafasi yake.

Wote mnakaribishwa.

kwa maelezo zaidi wasiliana nasi | +255653118018 | +255713197574 | +255672566076

IMETOLEWA NA:  
CHARLES F. ACHUODHO  
MKUU WA CHUO  
TAREHE: 23/10/2025